**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALIMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA**

SHULE YA SEKONDARI ISENYELA
S. L. P 145
**CHUNYA**
TAREHE04/12/2020.

KUMB.NA. ISS/C/UT.J/VOL.1

MWANAFUNZI..........................................................................
S.L.P 145.

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI ISENYELA MWAKA 2021.**

Uongozi wa shule ya sekondari Isenyela unayo furaha kubwa sana kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza. Shule iko katika kata ya mbugani wilayani Chunya. Iko umbali wa kilomita sita(6km) kaskazini mashariki mwa makao makuu ya wilaya kando ya barabara itokayo Tabora kwenda Mbeya mjini.

Shule itafunguliwa **tarehe 11/01/2021** hivyo unatakiwa kufika shuleni bila kukosa wala kuchelewa tarehe hiyo **saa 1:30 asubuhi** ukiwa na mzazi/mlezi wako. Mwisho wa kuripoti ni **tarehe18/01/2021** Baada ya hapo hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mzazi au mlezi ambaye mtoto wake hataripoti shuleni.

Nafasi uliyopewa ni bahati sana ,wapo wengi wangependa kupata lakini wameikosa, hivyo unatakiwa uitumie vizuri kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla.

Aidha unatakiwa kuzingatia kuwa wakati wote ukiwa mwanafunzi katika shule hii kigezo cha upimaji maendeleo yako itakuwa:- **NIDHAMU BORA, TAALUMA BORA na UTENDAJI WA KAZI ZA NJE**. Ukiwa shuleni nanje ya shule.

Pamoja na barua hii pokea,viambatanisho vifuatavyo:-

1. Sheria na kanuni za shule ambazo unatakiwa uzisome kwa makini na kuzielewa kisha uzifuate muda wote utakao kuwa mwanafunzi wa shule hii ndani na nje ya shule.
2. Orodha ya vifaa muhimu ambavyo lazima uje navyo shuleni
3. Fomu ya uthibitisho wa uraia wako,au nakala ya cheti cha kuzaliwa
4. Fomu ya uthibitisho wa afya yako
5. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na uongozi wa shule .
    - **Unatakiwa kuzikamilisha fomu hizi na kuzileta pamoja na barua hii ufikapo shuleni**



Scanned with CamScanner

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. **SARE ZA SHULE.**

WASICHANA

i. Sketi moja(1) ya malinda ( kitambaa cha **KIJANI JESHI** iliyo kolea na kiwe kizito)

ii. Sketi moja ya malinda kitambaa **CHEUSI** kizito, sketi zote ziwe ndefu, urefu sentimita 30 kutoka magotini kwenda chini.

iii. Mashati meupe mawili yenye kora , mikono mifupi.

iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba viwe na kisigino kifupi. **Sio bajaji, au simpo**

v. Sweta la rangi ya kijani jeshi shingo ya V na soksi nyeupe jozi mbili (2)

vi. Nguo za michezo mwanafunzi atazitumia wakati wa mazoezi. ( trackisut moja rangi ya dark blue )

**WAVULANA**

i Suruali mbili rangi **NYEUSI** moja na**KIJANI JESHI** moja, mashono mifuko miwili ya pembeni na mmoja wa nyuma upande wa kulia.**Suruali isiwe modo**

ii Mashati mawili (2) meupe yenye kora, mikono mifupi

iii Viatu vyeusi vya ngozi nyenye kamba na viwe na kisigino kifupi

iv Sweta rangi ya kijani jeshi shingo ya V

v Soksi za rangi nyeusi zaidi ya jozi mbili

vi. Nguo za michezo mwanafunzi atazitumia wakati wa michez( trackisut moja rangi ya dark blue )

**VIFAA VINGINE**

i Ndoo moja yenye ujazo wa lita kumi (10), kwaajili ya usafi.

ii Picha ndogo mbili (passpot size) kwaajili ya kuweka katika jalada la mwanafunzi kutunza kumbukumbu zake.

iii Jalada (file) moja kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake

iv Jembe moja lenye mpini (chapa kazi), fagio moja ndefu ya nje na mfupi mmoja wa ndani

v Aje na daftari kumi na mbili kaunta, mkebe, kalamu ya wino.

vi Hakikisha mwanafunzi ana mkoba/begi la shule kwaajili ya kubebea vifaa vyake

vii Mwanafunzi aje na kwanja moja kwa ajili ya usafi.

**"UONGOZI WA SHULE YA SEKONDARI ISENYELA UNAKUTAKIA UTEKELEZAJI MWEMA"**

**0767 271 730**



Scanned with CamScanner

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu **Na. 25 ya mwaka 1978**. Aidha inazingatia miongozo yote itolewayo na Wizara ya Elimu.

Hivyo shule kama jumuiya inapaswa iwe na taratibu ambazo jumuiya hiyo ili ifanikiwe katika kufanikisha malengo yake kwa ufanisizaidi.

Lengo la shule ni kufuta ujinga na pia kuwaandaa raia wema wa baadaye ili waweze kulitumikia Taifa katika sekta mbalimbali. Shule haitazamii kuandaa raia wa kuvunja sheria ( wahuni, wezi, majambazi, majangili, n.k)

### A. HESHIMA.

1. Kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa kuliko wako anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
2. Kutotumia lugha mbaya wakati wowote kwa wenzako, kwa mwalimu na kwa watu wengine.
3. Kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama walezi wako. Hivyo inakubidi uishi kwa amani na watu wote.
4. Kushirikiana na kusaidiana katika kazi zote ndani nanje ya darasa.
5. Kuheshimu na kuthamini kazi za aina zote.
6. Kila mwanafunzi anatakiwa kuitika mara moja na kukimbia aliko mwalimu/ mlezi au kiongozi anayemwita.
7. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, ofisi za shule, mali za shule au umma na za mtu binafsi. Endapo utafanya uharibifu wa aina yoyote utarudishwa kumwita mzazi ili afidie gharama husika.
8. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za serikali, Nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa.
9. Kusimama katika mstari ili kupata huduma kama wanaohudumiwa ni zaidi ya mtu mmoja.
10. Kila mwanafunzi awe mfano mzuri wa heshima na tabia njema popote awapo. Ni lazima wakati wote kuonesha nidhamu ya hali ya juu katika maongezi na mwalimu bila kutumia lugha chafu, kubishana, kukebehi au kuzomea au kuguna.
11. Nyoosha mkono unapotaka kujibu swali au kuuliza swali.
12. Unatakiwa kukaa kimya wakati wote uwapo darasani na usitoke nje ya darasa bila ruhusa.
13. Kila mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kukubali tofauti za kidini, kisiasa, na kiutamaduni zilizomo katika jamii.
14. Ni marufuku kufanya yafuatayo ukiwa shuleni nanje ya shule:
    - Kuvuta sigara
    - Kufuga kucha na kuwa na nywele zisizokuwa katika hali ya usafi.
    - Kufuga ndevu
    - Kuvaa mavazi yasiyokuwa ya heshima.
    - Kwa wavulana. Usinyoe kipara au kukata panki .



Scanned with CamScanner

- Kwa wasichana. Usipake rangi kucha, usisuke nywele, usivae sketi fupi na za kihuni wala kuweka dawa ya aina yoyote kwenye nywele, usipake wanja wala hina. USIJICHUBUE.
- Kugombana, kutukana, kupigana, au kuanzisha / kushiriki vurugu za aina yoyote na kuchochea kushiriki au kuanzisha mgomo.

**B. MAHUDHURIO**

Kila mwanafunzi;

(i) Ahudhurie muda wote wa masomo. Hatua kali zitachukuliwa kwa mzazi/mlezi atakaye mkalisha mtoto nyumani muda wa masomo.

(ii) Kuhudhuria *vipindi* vyote vya masomo *na kazi ya elimu ya kujitegemea*

(iii) Unaposikia wito wa dharula lazima kuheshimu kengele ya shule , hii ni pamoja na kuwahi sehemu yoyote unayotakiwa kuwa bila kuchelewa. Ukichelewa hatua za nidhamu zitachukuliwa dhidi yako.

(iv) Ufike shuleni kwa tarehe zilizopangwa tarehe ya kufungua shule iheshimike endapo mwanafunzi atachelewa kufika shuleni hatua za kisheria zitachukuliwa.

(v) Unatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama vile baraza la shule,ukaguzi wa usafi,kupandisha bendera ya Taifa, n.k

(vi) Unatakiwa kuhudhuria kazi zote za mikono zinazopangwa na shule.

(vii) Kutimiza kwa makini maandalio ya masomo yako ukiwa nyumbani.

**C. MIPAKA YA SHULE**

1. Wanafunzi wote wawepo ndani ya eneo la shule wakati wote wa shughuli za kishule zinapoendelea (masomo) isipokuwa kwa *kibali* maalumu kinachotolewa na mwalimu wa darasa/wa zamu/uongozi wa shule.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali:
    - Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu
    - Ofisi za shule
    - Maabara
3. Si ruhusa (ni marufuku) mwanafunzi kwenda kwenye:
    - Virabu vya pombe
    - Majumba ya starehe au kumbi za starehe
    - Nyumba za kufikia wageni (Guest House)
    - Pool table na kucheza

**D. USAFI**

- Usafi wa mwili
- Usafi wa sare za shule
- Usafi wa mazingira ya shule
- Usafi wa mazingira anayoishi



Scanned with CamScanner

- Usafi wa vyombo vya chakula
- Usafi wa kazi zake darasani

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati, ubakaji na ushoga
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani nan je ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi

HEADMISTRESS
ISENYELA SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 145
CHUNYA

**GERALD M. B.**
**MKUU WA SHULE**

***KARIBU SANA KATIKA SHULE HII YA ISENYELA***
***"ELIMU KWA MAENDELEO YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA"***



Scanned with CamScanner